

## HAVIFAIDI VIGARO

1. Awali ya vianziyo, nyuso huwa na mng'aro,  
Wazipanuwe tekeyo, waonekane wororo,  
Wafite wayafanzayo, tapo lao ni shambiro!  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.
2. Huja ichafuwe moyo, licha ya kwamba ni kero,  
Hao waiandamayo, waishishiliye ndaro,  
Japo ndiyo wapendayo, naona ina kasoro,  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.
3. Ya ujima tujwayo, hata kuwinda nguchiro,  
Hayo tuyaendeayo, tushikane pasi bero,  
Ela ngoma walo nayo, kuteza wapata ziro,  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.
4. Ushirika wa uchoyo, kazi kulishwa uporo,  
Na kuziandama nyayo, zingenga kwenye mitaro,  
Vyereje kushika mbiyo, uje bwagwa kwenye karo?  
Havifaidi vigaro, mavuniye ni matayo.
5. Na madomo ya mapayo, majisifu mkururo,  
Kukwimishwa bila wayo, mwambane "rero ni rero",  
Matusi uyapatayo, mtu utamani guro,  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.
6. Umoja ulo na pwayo, pa ng'ombe wapawa kuro,  
Uchao kutiwa gwayo, kwandamizwa makachero,  
Wapime uyatendayo, kana uwile mchoyo,  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.
7. Si ujamaa ni garo, kulimbikizwa mapyoro,  
Ahadi upatiwayo, si kitu vikorokoro!  
Wabaki ja mwele koyo, kwako ku giza totoro,  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.
8. Udhani mwenenda mbuyo, mliko mwasoza nchoro!  
Umwonaye mwema huyo, thomo waita nyinyoro,  
Si nyumba waliyo nayo, ni mfano wa danguro,  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.
9. Wangalimo koyokoyo, katika kinyang'anyiro,  
Sana kwao hizo ndeyo, na kutungiana vyero,  
Si hao waswubiriyo, hutanguliza charuro!  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.
10. Makuu wayaonayo, wauwangaza mkwiro,  
Dhamiri wailengayo, ule ule mnyororo,  
Mapigo wapitishwayo, waje kulipiza maro,  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.
11. Tamati ya niambayo, yazushayo migogoro,  
Mwanzowe wayashikayo, ja ndovu na wake mwiro,  
Haijawa ndowa hiyo, siyo ya kulisha soro!  
Havifaidi vigaro, mavunoye ni matayo.

***Omar Babu "Abu Marjan"***  
***Chuo Kikuu cha Ohio State***  
***Columbus, Ohio, Marekani***

---